**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI ILBORU**

**Simu: 0754985022**

**S. L. P 3014,**
**ARUSHA.**

---

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............**
**..................................................**
**S.L.P .........................................**
**.................................................**

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI ILBORU HALMASHAURI YA ARUSHA MKOA WA ARUSHA MWAKA 2024**

**1.0** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024/2025 na atasoma tahasusi ya HGL,/.PCM/PCB.......................

Shule ya Sekondari Ilboru ipo umbali wa Kilometa 02 Kaskazini mwa Mji wa Arusha Usafiri wa teksi/bajaji au bodaboda kutoka mjini unapatikana katika kituo kikuu cha mabasi. Nauli ni Shilingi 15,000 kwa teksi, kwa pikipiki ni Shilingi 3,000 na kwa bajaji ni shilingi 5,000.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 01/07/2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **.............** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **........**

**2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule:**

(i) Suruali (2) nyeusi Zenye marinda mawili kila upande.
(ii) Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali.
(iii) Mashati (2) meupe (tetron) ya mkono mirefu.
(iv) Tai ndefu 2 rangi nyeusi.
(v) Raba jozi 1 (flat) – Kwa jili ya michezo.
(vi) Nguo za michezo(jezi) rangi ya dark blue.
(vii) Bukta na T.shirt yennye mikono mifupi.
(viii) Sweta nyeusi moja yenye nembo ya shule shingo ya V.
(ix) Viatu vyeusi vyenye visigino vifupi vya kufunga na kamba(**sio buti**)
(x) Soksi jozi mbili nyeusi za shule.

**2.2 Nguo za kushindia (shamba dress).**

(i) Suruali ya kijivu cheusi mbili,upana wake ni inch 17 hadi 18 (kitambaa kimeambatanishwa),kama ukishindwa kutambua rangi uje shuleni utaelekezwa.
(ii) T-shirt mbili dark blue.(Unaweza kuzipata Jirani na shule)
(iii) Truck suit (1) light blue .(Unaweza kuzipata Jirani na shule)

**2.3 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

(i) Madaftari 12 yawe ni four or three quires
(ii) **Ream mbili (A4)** kwa mwaka .
(iii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika .
(iv) Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology.
(v) Scientific Calculator.
(vi) Godoro la sponji ft. 2 ½ (unaweza kuja kununulia Arusha).
(vii) Mashuka 2 light blue, blanketi 1, foronya 1, chandarua 1 (light blue).
(viii) Sabuni ya maji lita tano kwa matumizi ya usafi.
(ix) Nguo za ndani za kutosha.
(x) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe).
(xi) Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

**Wanafunzi waliochaguliwa kuja shule ya Ilboru wanatakiwa waje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya usafi wa mazingira.:-**

**VPCM** – Mifigio ya chelewa ya mpini mrefu -2, Soft broom- 1, Slesha -1, Jembe -1, Toilet brush- 1 na Squeezer- 1

**VPCB** - Soft broom-1, Slesha-1, Reki-1, Squiezer-1, Toilet rush-1 na mifagio ya chelewa ya mpini mirefu-2

**VHGL** - Toilet brush-1, jembe-1, Squiezer-1, Softbroom-1, Reki-1 na Hard broom-2

**2.4 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

- **Michango yote ni TShs. 80,000/=** Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule **Na.40801200237** katika **Benki ya NMB - ILBORU SEC. RECURRENT ACOUNT.** (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

**Sheria za Jumla:**

1. Kunywa pombe au kuvuta sigara au kiko ni mwiko.
2. Uzinifu wa aina yoyote ni kosa kubwa sana.
3. Kila mwanafunzi ni lazima awe mtiifu kwa walimu wake wote, wafanyakazi wote, makaka wa shule wote, na wakuu wengine wote. Ujeuri au ubishi wa aina yoyote kwa mwalimu, kaka wa shule au wakuu wengine wote ni mwiko.
4. Hakuna mwanafunzi yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya mipaka ya maeneo ya shule, bila ruhusa (pass) toka kwa mwalimu wa zamu, isipokuwa siku ya kuruhusiwa kwenda mjini rasmi (town leave). Mwalimu au kaka wa shule akimwona mwanafunzi yeyote mjini ana haki ya kumwomba amwonyeshe cheti cha ruhusa (pass).
5. Ruhusa ya kulala nje ya shule, itatolewa na Mkuu wa Shule au Makamu wake tu.
6. Kila mwanafunzi lazima aheshimu kazi za mikono zote ikiwa ni pamoja na bustani, usafi kama vile anavyopaswa kuheshimu masomo ya darasani.
7. Matusi ya aina yoyote, yawe ya kusema au kuandika hayaruhusiwi shuleni.
8. Kila mwanafunzi lazima aheshimu na kutunza mali ya shule, uharibifu wowote utakaotokea utabidi ugharimiwe na mwanafunzi mwenyewe.
9. Sare za shule (uniform) ni lazima zivaliwe wakati wa masomo na wakati wa kuruhusiwa kwenda mjini. Hakuna mwanafunzi yeyote atakayeruhusiwa kutoka nje ya mipaka ya shule bila kuvaa sare za shule, isipokuwa tu kama ruhusa rasmi imetolewa na Mkuu wa Shule.
10. Wizi wowote hauruhusiwi shuleni, iwe ni wa mali ya shule au mali ya mwanafunzi au mfanyakazi.
11. Usafi wa mwili, mavazi, madarasa, mabweni, jumba la chakula (dining hall) jumba la mikutano (assembly hall) jumba la mihadhara (lecture hall) viwanja ni wajibu wa kila mwanafunzi.
12. Ugomvi wa maneno au kupigana ni mwiko shuleni.
13. Kuchelewa kwa aina yoyote bila ruhusa ni kosa, mfano kuchelewa toka mjini, wakati wa roll-call, kuchelewa inspection na kuchelewa toka likizo.
14. Tabia njema shuleni na nje ya shule ni wajibu na ni lazima kwa kila mwanafunzi.
15. Taa za shule na maji ya shule lazima vitumiwe kwa uangalifu.
16. Magazeti au vitabu vyenye picha au maneno yasiyofaa havitakiwi shuleni.
17. Upokeaji au uandishi wa maneno yasiyofaa ni mwiko shuleni.
18. Mwanafunzi yeyote haruhusiwe kuandika barua yoyote kwa Mkuu yeyote mahali popote ya kiofisi bila ya kuipitisha kwa Mkuu wa Shule (k.k. Mkuu wa Shule).
19. Mwanafunzi yeyote haruhusiwe kwenda nyumbani kwa Mwalimu au Mfanyakazi yeyote bila ruhusa ya mwalimu anayehusika.
20. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kutumia vyombo vinavyotumia umeme kama vile redio, heater, pasi, earphone n.k. mabwenini au kufanya ufundi wa aina yoyote kwenye umeme bwenini au darasani.
21. Ili kuepukana na utoro, kofia **haziruhusiwi** hapa shuleni.
22. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya darasani pamoja na 'night preparation'
23. Ni kosa kupiga kelele Smart Area.
24. Ni kosa kugomea mitihani ya ndani na nje.
25. Ni kosa mwanafunzi kujihusisha au kushawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA:**

(i) Wizi
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
(iii)Kugoma na kuhamasisha mgomo
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule
(vi) Kukataa adhabu kwa makusudi
(vii) Kufuga ndevu
(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
(ix) Uvutaji wa sigara.
(x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa
(xi) Kukutwa au kitumia vifaa vya umeme kama vile, pasi hearter na n.k.
(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sharia za nchi.
(xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana au kushiriki kutoa mimba
(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
(xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu au kuwa na laini ya simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
(xvi) Kudharau Bendera ya Taifa
(xvii)Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
(xviii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.
(xix) Ni makosa mwanafunzi kujihusisha na dini (Kushawishi au kushawishiwa kubadili dini.

**4.0 Viambatisho na Fomu Muhimu**

(i) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
(ii) Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(iii)Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
(iv)Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
(v) **Result slip na Kivuli cha Cheti cha kuzaliwa.**
(vi)Stamp kwa ajili ya kutuma ripoti ya maendeleo ya kila muhula.
(vii) Sheria za shule za jumla.

**5.0** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

**KARIBU SANA .**

DENNIS J. OTIENO
MKUU WA SHULE
THE HEADMASTER
ILBORU SECONDARY SCHOOL
P. O. Box [illegible] ARUSHA

**MKUU WA SHULE**

**Mawasiliano mengine ya Shule.**

Namba za Simu ya shule: 0754090978
Mkuu wa Shule: 0754 985 022 /0621740533
Makamu Mkuu wa Shule: 0787411769/ 0753810559
Matron/Patron: 0767032368 /0782720622

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI ILBORU**

**Simu: 0754985022**

**S. L. P 3014,**
**ARUSHA.**

**08.07.2024**

**YAH: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ILBORU**

Nachukua nafasi hii kulishukuru Taifa letu kwa kunichagua na kunipa nafasi ya kupata Elimu ya Sekonari. Hii ni bahati kubwa na ninaahidi kujifunza kadiri ya uwezo wangu na sitapoteza muda wa masomo darasani au muda wa kazi za mikono kwa kuwa mvivu, au kupuuza shughuli hizo.

Nimesoma sheria za shule na masharti ya kujiunga na shule ya Sekondari Ilboru na ninakuthibitishia kuwa nimeafiki sheria na masharti hayo na kwamba nitaziheshimu kwa kutokuzivunja kwa makusudi. Na ikiwa nimezivunja ninastahili kuadhibiwa **vikali.**

Wako mwanafunzi mtiifu,

……………………………..

Jina na Sahihi ya Mwanafunzi

………………………………..

Jina na Sahihi ya Mzazi/Mlezi

***NB: (i) Wasilisha fomu hii kwa Mkuu wa Shule mara tu ufikapo shuleni ili iwekwe kwenye jalada lako.***

***PRESIDENT'S OFFICE***

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**(*To be completed by a medical Officer in respect of all form I and 5 entrants)***

Pupil's full name …………………………………………… Age…………………………………….

Blood count (red and white)
……………………………………………………………………………………………………
Stool examinations ……………………………………………………………………………
Urinalysis …………………………………………………………………………………………
Syphilis test ………………………………………………………………………………………
T.B.test ……………………………………………………………………………………………
Eyetest………………………………………………………………………………………………
Earstest ……………………………………………………………………………………………
Chest ………………………………………………………………………………………………
Abdomen ……………………………………………………………………………………………
Spleen ………………………………………………………………………………………………
Additional information: e.g. physical defects, infection, chronic or family diseases etc.
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
I certify that the above is fit to pursue further studies.

Signature ……………………………………….

Designation …………………………………..

Station …………………………………………

Date: …………………………………………..

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI ILBORU**

**S. L. P 3014,**
**ARUSHA.**

**Simu: 0754985022**

08.07.2024.

## FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina………………………………………………….
2. Dini ……………………………………….
3. Tarehe ya kuzaliwa…………………………
4. Kijiji ulimozaliwa………………….
4. Tarafa ulimozaliwa ………………… …….
5. Wilaya ulimozaliwa …………………
6. Mkoa ulimozaliwa …………………………. Kama unakaa mjini ……….
7. Taja mji:……………………………mtaa……………….barabara…………
8. Jina la baba……………………………. Kazi ya baba……………………….
9. Anwani ya baba………………………………………………………………………
10. Jina la mama ……………………………. Kazi ya mama……………….
11. Anwani ya mama …………………………………………………………………
12. Jina la atakayehusika na mwanafunzi kipindi chote cha masomo:
    Jina:…………………………………………………. Anwani:…………………………………
    Simu:…………………………………… Email: …………………………….
13. Shule ulizosoma madarasa madaraka uliyoshika

| Shule ulizosoma | madarasa | madaraka uliyoshika |
|---|---|---|
| …………………… | ………………… | ……………………………… |
| …………………… | ……………… | ………………………… |

14. Je, baba yu hai? ………………………………… (ndiyo/hapana)
15. Je, mama yu hai? ………………………………… (ndiyo/hapana)
16. Je, unakaa na mlezi ………………………… (ndiyo/hapana)
17. Anwani ya mlezi ……………………………………………………………
18. Kazi ya mlezi ……………………………………………………………
19. Eleza matatizo ya nyumbani, ya magonjwa, n.k. Yanayokukabili
    ……………………………………………………………………………………
20. Unafikiri matatizo hayo yatatatuliwa vipi?
    ……………………………………………………………………………
21. Eleza mipango yako ya maisha ya baadaye
    ……………………………………………………………………………………
22. Mko wangapi katika familia? (a) wa kiume ……………………………
    (b) wa kike ………………………. (c) wewe ni wa ngapi …………………
    (d) ndugu wangapi wameajiriwa? ……………………………………
23. Kazi ambazo ungependa kufanya baada ya kumaliza masomo
    ……………………………………………………………………………………
24. Kazi ambazo usingependa kufanya baada ya kumaliza masomo
    ……………………………………………………………………………………
25. Jina ………………………………. Sahihi…………….. Tarehe………………

**MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

Ukiwa mwanafunzi na mzazi/mlezi wamekubaliana na masharti yote ya shule, sharti fomu hii isainiwe na watu wanne, ambao ni:

(i) Mwanafunzi mwenyewe:

Jina kamili...................................................Kidato ....................Tarehe....................

(ii) Mzazi/Mlezi: Jina kamili ....................................Saini...................Tarehe....................

(iii) Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa: Jina la Kijiji/Mtaa..........................................................

(iv) Jina la Afisa Mtaa/Kijiji: .........................................................................................

Maoni/Mapendekezo kuhusiana na unavyomfahamu mwanafunzi huyu:
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................

Saini ya Afisa Mtendaji ............................................Tarehe............................

Mhuri wa Afisa Mtendaji:

(v) Mtendaji Kata/Mtaa: Jina la Kata/Mtaa...........................................................

Jina la Afisa Mtendaji Kata/Mtaa.................................................

Saini ya Afisa Mtendaji Kata ........................tarehe........................

Mhuri wa Afisa Mtendaji Kata:

**VITABU VYA KUJISOMEA**

Mzazi, unashauriwa kumnunulia mwanao vitabu muhimu vya rejea vifuatavyo:-

**MCHEPUO WA HGL**

(i) **HISTORY:**

(a) Norman Lowe – Mastering modern world history.
(b) Yassin Salehe – Essential in Advanced level history paper One and Two.

(ii) **GEOGRAPHY:** F. URIO (SUA) – SOIL
E. JOHN PRITCHARD – PRACTICAL GEOGRAPHY FOR AFRICA

(a) WAUGH, D – GEOGRAPHY, AN INTEGRATED APPROACH
(b) MORGAN - HUMAN ECONOMIC GEOGRAPHY
(c) BUNETT, R – PHYSICAL GEOGRAPHY
(d) MONKHOUSE – PRINCIPLES OF PHYSICAL GEOGRAPHY.

(iii) **LANGUAGE:**

(a) Advanced Dictionary of Contemporary English
(b) A practical approach 4th edition – Nicholaus Ashel.
(c) Advanced Level English – Oxford.
(d) Writing Skills – Kiura.

**VITABU VYA KUJISOMEA (PCB NA PCM ).**

(i) **PHYSICS:**

(a) Chand, S (2008) Principles Of Physics For Class x11 & x12, New Delhi.
(b) Nelkon & Parker (1995) Advanced Level Physics 7th Edition. Longman International Education.
(c) Duncan, T, New Understanding Physics for A-Level.

(ii) **CHEMISTRY:**

(a) Conceptual Chemistry – Chand S.K.
(b) Chemistry in Action – Michael Freematle
(c) Physical chemistry for A-Level and Undergraduate: Mkayuba and Ddungu.
(d) Soil and Environmental Chemistry.

(iii) **BIOLOGY:**

(a) Yaylor, D. J. (1997) Biological Science, Cambridge University Press.
(b) Susan Toole – Understanding Biology.
(c) Msaki, L (2003) Cell Structure.
(d) Msaki, L (2003) Systematics and Classification.

(iv) **MATHEMATICS:**

(a) Backhouse, Pure Mathematics 1
(b) Backhouse, Pure Mathematics 2
(c) Shayo Leonard, Advanced Mathematics Vol. I.
(d) Chand, S, Mathematics for Class xii.
(e) Understanding Mathematics.